TANGAZO LA SERIKALI NA. 50 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA SWAYA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Swaya ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 498 yenye majira-nukta 552589MS, 9012523KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 498A yenye majira-nukta 552356MS, 9011447KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA510 yenye

majira-nukta 554651MS, 9009940KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA509A, yenye majira-nukta 555935MS, 9007739KZ; hadi alama ya mpaka thence VMA509 yenye majira-nukta 556217MS, 9007353KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 505 yenye majira-nukta 554150MS, 9005673KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 3.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 506A yenye majira-nukta 552468MS, 9005086KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 6.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 506 yenye majira - nukta 547887MS,9008884KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 3.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 401 yenye majira-nukta 545449MS, 9009094KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba VMA 402 yenye majira-nukta 545057MS, 9008512KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 404 yenye majira-nukta 543850MS, 9010416KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 4.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 502 yenye majira-nukta 548098MS, 9011848KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 5.1.hadi ulipoanzia

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*